

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



S.L.P 42325,  
Simu Nambari: 2850633  
Nukushi: (022) 2850635  
Barua Pepe: [rbctemeke@pccb.go.tz](mailto:rbctemeke@pccb.go.tz)  
Wavuti: [www.pccb.go.tz](http://www.pccb.go.tz)

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**TEMEKE 29/06/2020**

**AFISA MTENDAJI MTAA WA KIZINGA AKAMATWA KWA RUSHWA**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Temeke jijini Dar Es Salam, imemkamata Karani wa Mahakama ya Mwanzo Temeke kwa kosa ya kuomba na kupokea Rushwa kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007.

Uchunguzi wa TAKUKURU ulibaini kwamba, mnamo tarehe 28/01/2020 SOPHIA HASHIMU MILLANZI ambaye ni Afisa Mtendaji Mtaa wa Kizinga Kata ya Mbagala, akiwa ofisini kwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kizinga alipokea fedha za mtego kiasi cha Shilingi 50,000/= ili aweze kumsaidia mwananchi mmoja (jina limehifadhiwa) kushugulikia mabadiliko ya jina la umiliki wa nyumba yaliyotokana mnada uliofanywa na benki ya NMB.

Uchunguzi dhidi ya tuhuma hii umekamilika na mtuhumiwa anatarajiwa kufikishwa mahakamani leo Jumatatu Juni 29, 2020 na kufunguliwa mashitaka kwa kosa la kushawishi, kuomba na kupokea rushwa kinyume na Kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na.11 ya mwaka 2007, katika Mahakama ya Wilaya ya Temeke.

TAKUKURU Mkoa wa Temeke inatoa wito kwa wananchi wote kuendelea kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kupitia mitandao yote ya simu kwa kupiga au kutuma ujumbe mfupi kwa namba ya bure 113 au kupiga 113 au kufuata maelekezo au fika katika ofisi ya TAKUKURU iliyopo karibu nawe.

**JENGA NCHI YAKO KATAA RUSHWA**

Imetolewa na:

**Donasian Kessy**

**Mkuu wa TAKUKURU (M)**

**Temeke**